



Panga mapema kama uko katika hatari kubwa ya ugonjwa mkali kutokana na COVID-19 na mafua (flu)

Je, uko katika hatari kubwa ya ugonjwa mkali kutokana na COVID-19 na mafua?

Hii inajumuisha:

- Watu wa umri wa miaka 60 na zaidi
- Wajawazito
- Watu wa Aboriginal, wa Visiwa vya Torres Strait na wa Visiwa vya Pasifika
- Watu wenye fetma, ugonjwa wa kisukari, ugonjwa mbaya wa moyo na mishipa, ugonjwa sugu wa mapafu (ikiwa ni pamoja na pumu kali inayohitaji kulazwa hospitalini katika miezi 12 iliyopita), ugonjwa sugu wa ini au wa figo, saratani au watu ambao wana kinga dhaifu
- Baadhi ya watu wenye ulemavu wakiwemo wale wenye ulemavu unaoathiri mapafu, moyo au mfumo wao wa kinga
- Wakazi wa vituo vya huduma ya wazee na ya walemavu
- Watu wa umri wa miaka 18 na zaidi ambao hawajachanjwa.

Kama ukiugua, daktari wako anaweza kupendekeza dawa ya kuzuia virusi ili kukusaidia kupata nafuu.

Utahitaji kutumia dawa hii haraka iwezekanavyo baada ya kuugua.

Panga mapema na zungumza na daktari wako sasa kama dawa ya kuzuia virusi ni sahihi kwako.

Ikiwa una matatizo yoyote ya kiafya na unahitaji usaidizi wa lugha piga simu kwenye TIS **131 450** na omba kwa NSW Health Flu na COVID-19 Care kwenye Home Support Line kwenye **1800 960 933**.

Tembelea www.nsw.gov.au kwa habari zaidi.